78

# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

## VETA

## CHUO CHA UFUNDI STADI NA HUDUMA VETA TABORA

MKATABA WA FUNDI UJENZI

**1.0 Maelezo ya mkataba**

i) Jina la mkataba: - KAZI YA KUWEKA TERAZZO JENGO LA STOO.

ii) Na. ya mkataba: VETA/TBR/UYUI/DVTC/PHASE II/GSTORE/10.

**2.0 Makubaliano:**

Makubaliano haya yamefanyika leo siku ya JUMANNE Tarehe 19 mwezi 4 Mwaka 2022 Kati ya Mkuu wa Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma VETA Tabora (Tabora RVTSC) wa S. L. P. 2060 Tabora, ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 802 Dodoma (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

Bw. **Emmanuel Ezekekiel Lubona** wa S. L. P. 161, Tabora (ambaye hapa anatambulika kama Fundi).

Kwamba mwajiri anampatia Fundi kazi ya uwekaji terrazzo katika jengo la stoo (general store)

Kwamba kazi hii itafanyika katika eneo la chuo cha Ufundi cha Wilaya ya Uyui lililopo eneo la Idete mkabala na shule ya sekondari ya Idete, Wilaya ya Uyui katika mkoa wa Tabora.

Gharama ya kazi hii ni jumla ya **Shilingi 800,000.00** Kwa maneno, **(Shilingi Laki nane tu).**

Kwamba kazi hii itachukua muda wa siku ......... kwa maneno ( ................................) mpaka kukamilika.

**3.0 Mwajiri:**

Kwamba mwajiri amekubali gharama iliyotolewa na Fundi kwa kazi iliyotajwa hapo juu.

**4.0 Fundi:**

Fundi amekubali kuifanya kazi hiyo kwa kusimamiwa na Msimamizi wa ujenzi pamoja na kamati ya ujenzi kwa gharama iliyoelezwa hapo juu na kuikamilisha kwa siku zilizotajwa hapo juu.

**5.0 Mwajiri na Fundi kwa pamoja wamekubaliana:**

i Kwamba kazi itafanyika kwa kiwango cha hali ya juu kwa mujibu wa viwango vya majengo ya serikali.

ii Kwamba kabla ya malipo kazi itakaguliwa na Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui aliyeteuliwa kukagua kazi za ujenzi wa chuo cha ufundi cha Wilaya ya Uyui.

iii Kwamba Fundi hataendelea na hatua nyingine ya ujenzi mpaka hatua ya awali imekaguliwa na kukubalika na Mhandisi wa Wilaya na kamati ya ujenzi.

iv Kwamba iwapo itabainika kwamba Fundi amejenga kinyume na maelekezo ya Msimamizi wa ujenzi, Fundi atawajibika kubomoa na kurekebisha kwa gharama zake.

v Kwamba malipo yatalipwa pale tu ambapo awamu husika ya ujenzi imekamilika na imekaguliwa na Mhandisi wa Wilaya ya Uyui pamoja na kamati ya ujenzi na kuthibitishwa kwa maandishi.

vi Kwamba malipo yote yatafanywa kupitia mfumo wa malipo serikalini (MUSE) kwa hiyo Fundi anatakiwa kuwa na akaunti benki.

vii Kwamba endapo itabainika kuwa Fundi anakiuka mashariti ya mkataba huu bila sababu za msingi, uongozi wa chuo cha ufundi VETA Tabora utafuta/utavunja mkataba huu na Fundi hatalipwa chochote na hatua za kisheria zitachukuliwa.

ViiiMalipo yote yatakatwa kodi ya zuio ya asilimia tano (Withholding Tax 5%) kama sheria za kodi zinavyosema.

## 6.0 Fedha ya zuio (retention fund)

Mwishoni mwa kazi iliyoanishwa katika Mkataba huu, Mwajiri atabaki na 5% ya gharama ya ujenzi hadi pale muda wa matazamio ya ujenzi (miezi sita) utakapokwisha. Fedha hizo zinaweza kutumika pale tu ambapo kuna uharibifu umetokea katika ujenzi ndani ya kipindi cha matazamio ya ujenzi na Fundi akashindwa au akakataa kurekebisha uharibifu huo ndani ya muda wa majuma mawili (2) baada ya kupata maelekezo ya Mwajiri.

## 7.0 Nyaraka zinazokamilisha mkataba huu ni:

- Hati za bei za Fundi
- Michoro na vipimo vya majengo
- Barua ya kukubali kazi ya Fundi
- Mkataba wenyewe

## 8.0 Saini za pande zote mbili:

Imetiwa saini na

**MWAJIRI**

Jina: DKT. KYOMO, Z.B.

Cheo: MKUU WA CHUO

Saini: ..............................

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UFUNDI NA HUDUMA
TABORA

**SHAHIDI**

Jina: JAPHARY B. MWAMBETE

Cheo: AFISA UGAVI

Saini: ..............................

**FUNDI**

Jina: Emmanuel E. Lubona

Saini: ..............................

**SHAHIDI**

Jina: Ayoub M. Christopher

Saini: ..............................

copy

# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

## VETA

## CHUO CHA UFUNDI STADI NA HUDUMA VETA TABORA

MKATABA WA FUNDI UJENZI

(NYONGEZA YA MKATABA)

**1.0 Maelezo ya mkataba**

**Hii ni nyongeza ya Mkataba**

i) Jina la mkataba: – KUJENGA JENGO LA GENERA STORE

ii) Na. ya mkataba: VETA/TBR/UYUI/DVTC/CONSTRUCTION/GENERAL/STORE/02

**2.0 Makubaliano:**

Makubaliano haya ya nyongeza ya mkataba yamefanyika leo siku ya ALHAMIS Tarehe 16 mwezi PILI Mwaka 2022 Kati ya Mkuu wa chuo cha ufundi na huduma VETA Tabora (Tabora RVTSC) wa S. L. P. 2060 Tabora. (ambaye hapa anatambulika kama Mwajiri)

NA

Bw **EMMANUEL EZEKIEL LUBONA** wa S. L. P. 161 (ambaye hapa anatambulika kama Fundi).

Katika mkataba huu zimeongezwa kazi za kuweka mfumo wa maji safi na maji taka kwa jendo lote la General Store kwa gharama ya **Tsh. 150,000.00 (Laki moja na elfu hamsini tu)**

Kwamba kazi hizi zitachukua muda wa siku 16 (siku ALHAMIS 13/3/2022)

Mashariti na vigezo vya kazi hii ya nyongeza vinabaki kama mkataba Na: VETA/TBR/UYUI/DVTC/CONSTRUCTION/GENERAL/STORE/02 unavyosema.

**3.0 Saini za pande zote mbili:**

Imetiwa saini na

**MWAJIRI**

Jina: DKT. Kyomo, Z.B.

Cheo: Mkuu wa Chuo

Saini: ..........

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UFUNDI NA HUDUMA
TABORA

**SHAHIDI**

Jina: JEPHARY B. MWAMBETE

Cheo: HRAO

Saini: ..........

**FUNDI**

Jina: Emmanuel. Lubona

Saini: ..........

**SHAHIDI**

Jina: Neema S. Kisogoa

Saini: ..........